

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA PILI

KIKAO CHA SABA

10 FEBRUARI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA PILI

KIKAO CHA SABA – TAREHE 10 FEBRUARI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Taarifa ya Mwaka ya Benki Kuu ya Tanzania kwa Mwaka 2019/2020 (*The Annual Report of Bank of Tanzania for the year 2019/2020*).

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha Mapitio ya Nusu Mwaka, 2020/2021 (*Monetary Policy Statement: The Mid-Year Review 2020/2021*).

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

88. MHESHIMIWA JAFARI WAMBURA CHEGE (RORYA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Daraja la Mto Mori; kwani Mto huo umekuwa ukisomba Watu na kusababisha vifo kwa Wananchi wanaofuata huduma upande wa pili.

89. MHESHIMIWA ASIA ABDULKARIM HALAMGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni Halmashauri ngapi nchini zimeteteleza kwa asilimia 100 Sheria ya utoaji mikopo asilimia 10 ya makusanyo ya ndani kwa makundi ya Vijana, Akina Mama na Watu wenye mahitaji maalum.

90. MHESHIMIWA SILVESTRY FRANCIS KOKA (KIBAHA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Miundombinu ya maji katika Shirika la Elimu Kibaha ilijengwa miaka 50 iliyopita kwa kutumia mabomba ya asbesto ambayo siyo rafiki kwa afya ya binadamu; lakini pia ni chakavu sana:-

- (a) Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya maji katika Shirika hilo.
- (b) Je, ni lini Serikali itakarabati majengo ya Chuo cha FDC katika Shirika hilo.

**91. MHESHIMIWA DKT. DAVID MATHAYO DAVID
(SAME MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini utekelezaji wa ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne ya kujenga Daraja la Mto Pangani mpakani mwa Wilaya za Same na Simanjiro utaanza.

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

**92. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY
(MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini minara ya simu itajengwa katika Kata za Endahagichen – Ndamilay, Mewadan – Magong na Endaghadat – Qamtananat katika Jimbo la Mbulu Vijijini ambazo hazina mawasiliano ya simu.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

93. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-


Je, ni lini Serikali itafufua viwanda vyote vya kubangua Korosho vilivyopo Manispaa ya Mtwara Mikindani.

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

94. MHESHIMIWA AUGUSTINE VUMA HOLLE (KASULU VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua mgogoro wa ardhi kati ya Kijiji cha Mgombe na Kambi ya Jeshi Mtabila.



WIZARA YA NISHATI:



95. MHESHIMIWA ALOYCE JOHN KAMAMBA (BUYUNGU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

- (a) Je, ni kwa nini baadhi ya Vijiji vya Wilaya ya Kakonko havijapata umeme;
- (b) Je, ni lini sasa Vijiji hivyo vitapata umeme.

WIZARA YA KILIMO:

**96. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON
MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-
Serikali imezuia Kampuni binafsi kununua
Kokoa katika Wilaya za Kyela na Rungwe kwa
msimu huu na Vyama vya Ushirika havina
uwezo wa kununua Kokoa hizo kwa Wananchi:-

Je, ni lini Serikali itaruhusu tena Kampuni binafsi
kuendelea kununua Kokoa.

**97. MHESHIMIWA ALLY ANYIGULILE MLAGHILA
(KYELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-
Mfumo wa stakabadhi ghalani kwa zao la Kokoa
haujamnufaisha Mkulima:-

Je, ni lini sasa mfumo huo utabadilishwa ili
kukidhi lengo la Ushirika.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**98. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH
SHANGAZI (MLALO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na
Uchukuzi:-


Je, ni lini ahadi ya Serikali ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Lushoto – Muyanta hadi Mlalo itaanza kutekelezwa.

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

99. MHESHIMIWA MWANTUM MZAMILI ZODO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na upungufu wa Watumishi wapatao 16,000 kwenye Sekta ya Afya nchini.



WIZARA YA MAJI:

100. MHESHIMIWA ANTON ALBERT MWANTONA (RUNGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Serikali ilifanya upembuzi yakinifu na kubaini kuwa jumla ya shilingi Bilion 21 zinahitajika ili kukarabati miundombinu ya maji Mji wa Tukuyu:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha na kuanza ukarabati wa miundombinu hiyo.

**101. MHESHIMIWA ENG. EZRA JOHN
CHIWELESA (BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa mradi wa kutoa maji toka Ziwa Victoria kuyapeleka Biharamulo kama Mhe. Rais alivyoahidi tarehe 16/09/2020 alipokuwa Biharamulo katika Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

**102. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA
SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-
• Serikali iliahidi kufikisha Urambo Maji ya Ziwa Victoria na kwa sasa yameshafika Tabora:-

- (a) Je, ni hatua zipi zimechukuliwa katika kutekeleza azma hiyo;
- (b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa katika mwaka huu wa fedha, na ni lini maji yatafika Urambo.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge sasa lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 –

2025/26) na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2021/22 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/22.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
10 FEBRUARI, 2021**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**

